



# TAARIFA YA MKUTANO MKUU MAALUM WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu Maalum wa Wanahisa wa Shirika la Ndege la Precision Air utafanyika siku ya Ijumaa Tarehe 21 mwezi Machi 2025 katika Ukumbi wa Mkutano wa Kilimanjaro A, Jengo la Ubungo Plaza, Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam, kuanzia saa Tatu kamili Asubuhi.

## Ajenda ya Mkutano itakua kama ifuatavyo:

1. Kufungua Mkutano
2. Kupitisha Ajenda za Mkutano
3. Kupokea na kupitisha Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi, Taarifa ya Hesabu za Fedha na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018, 2019, 2020, 2021, 2022 na 2023.
4. Kupitisha uteuzi wa Wakurugenzi Pamoja na malipo yao kwa kipindi cha mwaka 2019 - 2024
5. Kupitisha uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa kipindi cha mwaka 2019 - 2024
6. Kupokea na kuidhinisha mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Uendeshaji wa kampuni (MEMARTS) kuruhusu Mkutano Mkuu wa Wanahisa kufanyika kwa njia ya mtandao.
7. Mengineyo
8. Kufunga Mkutano.

## Mambo ya Kuzingatia

1. Orodha (Register) ya Wanahisa watakaostahili kupiga kura itafungwa Jumanne tarehe 18 Machi, 2025, saa Nane Mchana.
2. Mwanahisa atajigharamia gharama za kuhudhuria Mkutano na atatakiwa kufika kwenye Mkutano akiwa na nakala yake ya Risiti ya Uwekezaji wa Hisa (Depositary receipt), pamoja na kitambulisho chochote kati ya hizi:- Hati ya Kusafiria (Passport), Kitambulisho cha Taifa (NIDA), Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Mpiga Kura.
3. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni. Nakala ya fomu ya uwakilishi iliyosainiwa na Mwanahisa ifikishwe katika ofisi za Kampuni zilizopo: Ghorofa ya Kwanza jengo la Diamond Plaza, Makutano ya Barabara za Mirambo na Samora, Dar es Salaam au itumwe kwa barua pepe Kwenda: **[pwmanagement@precisionairtz.com](mailto:pwmanagement@precisionairtz.com)** kabla ya saa Nane Mchana, Jumanne tarehe 18 Machi, 2025.
4. Nakala za Makabrasha ya Mkutano Pamoja na Fomu ya Ukawakilishi zitapatikana katika tovuti ifuatayo ya Kampuni: (**<https://www.precisionairtz.com/about-us/investor-relations>**).
5. Taarifa yoyote itakayojadiliwa chini ya Ajenda Namba. 7 itatakiwa kupokelewa na katibu wa kampuni kwa njia ya maandishi kabla ya saa Nane Mchana, Ijumaa tarehe 07 Machi, 2025.

Notisi hii na Ajenda ya Mkutano zimetolewa Dar es Salaam leo tarehe 28 Februari, 2025

**MIGIRE KEMBO MIGIRE**

**KATIBU WA KAMPUNI**

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**